# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

***Dodoma***
***03 Februari, 2024***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI MIKATABA YA UENDESHAJI WA KITALU CHA MNAZI BAY**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Nishati kuhakikisha sekta ya gesi asilia inakidhi mahitaji kwa bei nafuu ili itumike nyumbani, viwandani na kwenye vyombo vya usafiri.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati wa hafla ya utiaji saini mauziano ya hisa za kampuni ya ***Wentworth Resources Plc*** katika kitalu cha Mnazi Bay baina ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kampuni ya ***Maurel & Prom (M&P).***

Aidha, Rais Samia amesema mabadiliko ya tabianchi yamefanya mahitaji ya gesi na nishati nyingine mbadala kuwa kipaumbele katika kujenga uchumi shindani hivyo wizara haina budi kuongeza uzalishaji na usambazaji.

Vile vile Rais Samia amesema serikali inaendelea kufanya jitihada maalum kuhakikisha rasilimali za nchi ikiwemo gesi asilia zinawanufaisha wananchi na Taifa kikamilifu.

Rais Samia pia amesema shabaha ya serikali ni kuendelea kunufaika zaidi na gesi asilia kwa kuhamasisha uzalishaji zaidi kwenye visima ambavyo tayari gesi imeshagundulika.

Hali kadhalika, Rais Samia amebainisha kuwa gharama za kuendeleza miradi ya gesi ni kubwa hivyo huilazimu serikali kuingia ubia na sekta binafsi ambao wana mitaji, ujuzi na teknolojia ya kisasa.

Ununuzi wa hisa hizo utasaidia kuongeza mapato kwa TPDC na serikali, kuimarisha usalama wa nishati nchini kwa kuepuka sehemu kubwa ya kitalu kumilikiwa na kuendeshwa na kampuni moja.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu